



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA. *KAPT*
(MST) GEORGE H. MKUCHIKA (Mb.), AKIWASILISHA BUNGENI
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA
FEDHA 2019/20**

APRILI, 2019

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09), na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04). Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20.

2. Mheshimiwa Spika, Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uwezo wa kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ninamuahidi kuwa nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Newala Mjini kwa ujumla kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapoe ndelea kuwawakilisha. Vile vile, naishukuru familia yangu ushirikiano wanaonipatia na kwa kuwa wavumilivu ninapote keleza majukumu ya taifa. Aidha, napenda kumpongeza Dkt. Mary M. Mwanjelwa (Mb.) kwa kuteuliwa kwake na pia namshukuru kwa kunisaidia katika kazi za kila siku za kuiongoza ofisi yangu.

3. Mheshimiwa Spika, Naomba kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kuendelea na nafasi zao. Pia, nawapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa na wanaoendelea katika nafasi zao zenye dhamana ya kusimamia Kamati katika kuishauri Serikali na kutoa mapendekezo mbalimbali ya kuboresha utendaji kazi. Vilevile nawapongeza wajumbe wapya wa kamati yetu, Mheshimiwa Ibrahim Hasanali Raza (Mb), Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Njalu Saudi Silanga (Mb), Philipo Mulugo (Mb) na Mheshimiwa Mansoor Hirani Shanif (Mb).

4. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake

Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum Tabora kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2018/19 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20. Maoni na ushauri wa Kamati hiyo yametuwzesha na yataendelea kutuwzesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

5. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaohimiza uadilifu, uwajibikaji, uchapakazi na utendaji wenye matokeo katika Utumishi wa Umma na usimamizi wa miradi mikubwa ya kimkakati kwa Taifa. Pili, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

6. Mheshimiwa Spika, Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar na kuimarisha Muungano, amani na utulivu. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa ushupavu na uadilifu mkubwa.

7. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa nguzo muhimu ya utekelezaji, usimamiaji na uratibu wa kazi za kila siku za Serikali na kuwa Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Aidha, napenda kumpongeza kwa uratibu makini wa kufanikisha zoezi la Serikali kuhamia Dodoma hasa ujenzi wa ofisi mpya kwenye Mji wa Serikali.

8. Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa umahiri na kazi nzuri wanayoifanya ya kukusaidia wewe kuliongoza Bunge letu Tukufu.

9. Mheshimiwa Spika, Nawapongeza pia Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio wanayoendelea kuyapata katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Kwa namna ya pekee, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Selemani Said Jafo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Mheshimiwa Mwita Waitara (Mb) na Mheshimiwa Joseph Kandege (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

10. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa hivi karibuni ambao ni Mheshimiwa Christopher Kajoro Chizza kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Korogwe Vijijini, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Liwale, Mheshimiwa James Kinyasi Millya kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, Mheshimiwa Ryoba Chacha Marwa kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Serengeti, Mheshimiwa Paulina Philip Gekul kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Temeke. Vile vile, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa msiba wa Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Korogwe Vijijini kilichotokea tarehe 2 Julai, 2018. Tunaomba Mola aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina!

11. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Joseph George Kakunda (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga (Mb.) kuteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anjellah Kairuki (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Mheshimiwa Doto Biteko (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, na Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Kabudi (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Mary Machuche Mwanjelwa (Mb.) kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu (MB) kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maliasili

na Utalii, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb.) kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa (Mb.) kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Wote hao nawatakia mafanikio katika nafasi walizopewa na Mheshimiwa Rais.

12. Mheshimiwa Spika, nawashukuru Balozi Mhandisi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Dkt Moses Kusiluka Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean J. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Dkt Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati.

13. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuzishukuru na kuzitaja nchi chache ambao ni:- Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Korea ya Kusini, Ujerumani, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Indonesia, Brazil, Italia, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ireland, Israel, Kenya, Rwanda, Somalia, Afrika Kusini, Botswana, Msumbiji, Malawi, Mali, Ghana, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Nigeria, Sierra Leone, Liberia, Ivory Coast, Namibia, Niger, Togo, Zimbabwe, Trinidad & Tobago na Ubelgiji. Vilevile, nawashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, OFID-OPEC Fund for International Development, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan (Japanese Social Development Fund), DfID, KOICA, GIZ, DFATD, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, NORAD, JICA, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

14. Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa. Uzalendo wao na imani yao kwa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano umewezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi, kwa ufanisi mkubwa.

15. Mheshimiwa Spika, naomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

itaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nyakati mbalimbali kuhusu kupunguza urasimu ili kuongeza kasi ya utekelezaji, kubana matumizi na kurejesha nidhamu ya Serikali na Utumishi wa Umma kwa kuongeza uwazi na kusimamia Sheria, Kanuni Miongozo na Taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike kwa wananchi ambao ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma. Vilevile, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu wa mali ya umma, ufisadi, uzembe, uvivu, ukiukwaji wa maadili na watumishi hewa na wasio na sifa stahiki kwa kuwawajibisha wanaodhihirika kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazoendelea kuchukua Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu pamoja na wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Serikali inayowahudumia wananchi wa kawaida itatimia kwa watumishi wa umma wote kufanya kazi kwa weledi, juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. Tunaendelea kusisitiza utoaji wa huduma bora, kwa haraka na kwa staha ili kuwaondolea wananchi usumbufu.

16. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu, Viongozi na Watumishi wa umma waliopoteza maisha yao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki ikiwemo ajali za Magari kwa watumishi wa umma waliofariki wakiwa kazini tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

17. Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni: Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 pamoja na Mpango wa Utekelezaji na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20.

A. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2018/19

18. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015. Shughuli zilizotekelezwa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

3.1 OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

19. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu ilidhinishiwa **Shilingi 22,644,912,748** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2019 **Shilingi 16,131,509,229** zilipokelewa na kutumika.

20. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (Fungu 30) inayojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhinishiwa **Shilingi 576,213,769,000**.

Kati ya fedha hizo, Shilingi **401,158,280,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 175,055,489,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2019 **Shilingi 427,830,330,741** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 304,632,948,634** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 123,197,382,107** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo kwa kila Taasisi:-

21. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

- (i) Huduma ziliendelea kutolewa kwa Mhe. Rais na familia yake.
- (ii) Ushauri umeendelea kutolewa kwa Mhe. Rais kuhusu ratiba ya kila siku.
- (iii) Ushauri umeendelea kutolewa kwa Mhe. Rais katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia na ushauri mwingine wowote wenye lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi.
- (iv) Mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 59 zilichambuliwa. Mikutano 12 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 18 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano tisa (9) ya kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada 20 ziliwasilishwa na kujadiliwa. Mikutano mitano (5) ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 14 zilijadiliwa na kufanyiwa maamuzi. Aidha, mikutano minne (4) ya Kamati ya Katiba na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo miswada 16 ilijadiliwa
- (v) Vikao vya Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri ya Uratibu wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (2017 - 2022) vilifanyika tarehe 24 Agosti, 2018 na tarehe 26 Oktoba, 2018 Dar es Salaam;
- (vi) Rufaa 124 za Watumishi wa Umma, Mamlaka ya Nidhamu na Waajiri zilichambuliwa na kutolewa uamuzi na Rais na Katibu Mkuu Kiongozi ambapo wahusika walijulishwa. Aidha, malalamiko 689 ya Watumishi wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo; na
- (vii) Ufuatiliaji umefanyika katika uandaaji wa Programu za Maboresho za Serikali za Mitaa (LGRP), Maboresho katika Utumishi wa Umma (PSRP) na Maboresho katika Sekta ya Sheria (LSRP).

22. Mheshimiwa Spika, kazi nyinginezo zilizotekelezwa katika fungu hili zipo katika ukurasa wa 10 hadi 14 wa Kitabu cha Hotuba.

3.1.1 TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

23. Mheshimiwa Spika, Matokeo ya juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mh. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli katika kukabiliana na rushwa nchini zimeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza nidhamu na uwajibikaji wa watumishi wa umma, kujengeka kwa uadilifu katika biashara, ukusanyaji mapato na matumizi ya umma. Mafanikio haya yameijengea Serikali msingi/uwezo mpana wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma za msingi kwa wananchi wake.

24. Mheshimiwa Spika, Taarifa mbali mbali zinazotolewa na taasisi za kimataifa na za kitaifa kuhusiana na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika mapambano dhidi ya Rushwa zimedhihirisha Tanzania inapiga hatua kubwa katika kudhibiti vitendo vya rushwa na ufisadi nchini.

25. Mheshimiwa Spika, Kiashiria cha **Transparency International (CPI)** kimeonesha kuwa kwa mwaka 2018, Tanzania imefanya vizuri kwa kiwango cha juu ya wastani ukilinganisha na nchi nyingine za Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kufikia kiwango cha asilimia **36** na kushika nafasi ya **99** kati ya nchi **180** ikilinganishwa na nafasi ya **103** ya mwaka **2017**. Aidha, kwa kutumia kiashiria cha **Mo Ibrahim**, kiashiria kinaonesha kuwa Tanzania ilipiga hatua katika nyanja ya Utawala Bora kwa kupata asilimia **58.5** ikilinganishwa na asilimia **57.5** ya kiwango kilichofikiwa mwaka **2016**

26. Mheshimiwa Spika, Utafiti uliofanywa na **AFROBAROMETER** mwaka 2014 ulionesha kuwa asilimia **66** ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa kimeongezeka. Hata hivyo, matokeo ya utafiti uliofanyika wa mwaka **2017** yanaonesha kuwa asilimia **72** ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa kimepungua. Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa na **TWAZEZA** mwaka **2017** nao umebainisha kuwa asilimia **85** ya wananchi waliohojiwa walieleza kuwa rushwa imepungua ukilinganisha na asilimia **11** ya waliohojiwa mwaka **2014**.

27. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

- (i) Uchunguzi wa majalada 170 ulikamilika na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuombewa kibali. Majalada 107 kati ya yaliyopelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Aidha, majalada mengine yanaendelea kufanyiwa kazi
- (ii) Shilingi milioni 977.92 ziliokolewa kutokana na operesheni zilizofanywa na TAKUKURU na kurejeshwa serikalini kutokana na kudhibiti rushwa katika eneo la ukusanyaji mapato ya Serikali, uzuiaji wa malipo hewa na ukaguzi wa miradi ya maendeleo;
- (iii) Elimu kuhusu athari za rushwa na juhudi za Serikali za kuidhibiti ili kupata uungwaji mkono ilitolewa kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina, mikutano ya hadhara, vipindi vya redio na Runinga,

maonesho, vyombo vya habari pamoja na kusambaza makala na machapisho yanayohusu athari za rushwa.

- (iv) Kufuatia utekelezaji mzuri uliofanyika katika vita dhidi ya rushwa kupitia TAKUKURU uungwaji mkono unatakiwa kwa kila mdau; hivyo natoa rai kwa Taasisi za Umma kuwaalika kwenye mikusanyiko mbali mbali kama semina, warsha na mikutano ili elimu dhidi ya rushwa iwe ya hali ya juu nchi nzima. Kwa taasisi za umma haya ni maelekezo ya Serikali. Aidha, wadau wengine wanaaswa kuwaalika TAKUKURU kwenye mikutano ama semina zao ili kupata elimu hiyo.

28. *Mheshimiwa Spika*, Kazi nyinginezo zilizotekelezwa zipo katika ukurasa 14 hadi 21 wa Kitabu cha Hotuba.

3.1.2 TAASISI YA UONGOZI

29. *Mheshimiwa Spika*, Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha utaalum wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

30. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2018/19, kwa muhtasari kazi zifuatazo zimetetelezwa:-

- (i) Kozi saba (7) za muda mfupi zimetolewa kwa Viongozi wa Umma 431 kwa lengo la kuimarisha utendaji wao. Kozi hizi ni kwenye maeneo ya Uongozi wa kimkakati; Utawala; Mitazamo na Dira; Kiongozi Muadilifu; Uongozi Binafsi na Wenye Maadili; Mapambano Dhidi ya Rushwa, Utawala Bora na Uwajibikaji; Usimamizi wa Mipango yenye Matokeo; na Huduma kwa wateja na
- (ii) Mafunzo ya kuwajengea uwezo Viongozi wa kisiasa na watendaji wa Serikali katika ngazi za Mkoa na Wilaya yalitolewa ambayo matokeo yake yameonekana kwa kupungua kwa maamuzi yasiyozingatia sheria, kanuni na maadili ya nafasi za wateule.

31. *Mheshimiwa Spika*, taarifa kwa kina ipo katika kitabu cha Hotuba ukurasa wa 21 hadi 27 wa Hotuba yangu.

3.1.3 MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

32. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) umeendelea kutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa Biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, MKURABITA imejenga uwezo Vyama vya wakulima uwezo wa kutumia Hati Miliki za Kimila kupata Mitaji katika Benki na Taasisi nyinginezo za Fedha.

33. Mheshimiwa Spika, Kazi nyingine za MKURABITA zilizotekelezwa zipo katika ukurasa 27 hadi 31 wa Kitabu cha Hotuba.

3.1.4 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

34. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; takwimu zinaonesha kwamba asilimia 28.2 ya Watanzania ni maskini. Serikali ya Awamu ya Tano imepata mafanikio kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao umewezesha kuzikwamua kaya maskini milioni 1.1 zenye walengwa zaidi ya milioni 5 ambayo ni karibu asilimia 40 ya maskini wa kipato. Ili kufanikisha hilo TASAF imehawilisha pesa kwa masharti ya kuboresha lishe, elimu na afya. Vile vile, TASAF imeendesha mpango wa kutoa ajira za muda ili kuongeza kipato na kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza kwenye shughuli za kiuchumi kwa lengo la kukuza uchumi wa kaya. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 baadhi yaliyofanyika ni kama ifuatavyo:

- (i) Ruzuku ya jumla ya Shilingi bilioni 163.5 ilihawilishwa kwa kaya maskini 1,007,588 zilizoandikishwa zenye jumla ya watu zaidi ya milioni 5 Tanzania Bara na Zanzibar katika Vijiji/Mitaa/Shehia 9,835. Kaya hizo zimeweza kupata ruzuku hiyo kwa masharti ya lishe, afya na elimu; na
- (ii) Mpango wa kutoa ajira za muda umetekeleza miradi 3,567 kutoka katika Vijiji, Mitaa na Shehia zipatazo 2,590 ambapo kaya za walengwa 288,837 zilipata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar. Miradi hiyo ina thamani ya Shilingi bilioni 15.1. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti, uchimbaji wa visima vifupi, uboreshaji wa barabara, uhifadhi wa vyanzo vya maji, na hifadhi ya mazingira. Aidha, watoa huduma 152 wa ngazi ya jamii wamefundishwa namna ya kusimamia miradi ya kutoa ajira za muda katika Maeneo 19 ya Utekelezaji;

35. Mheshimiwa Spika, Kazi nyinginezo zilizotekelezwa katika kipindi hicho zipo katika ukurasa wa 31 hadi 37 wa Kitabu cha Hotuba.

3.1.5 MFUKO WA RAIS WA KUJITEGEMEA

36. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umetoa huduma mbalimbali ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Aidha, mfuko huu utakamilisha kazi zake katika mwaka huu wa fedha na hautakuwepo kwa mwaka wa 2019/20.

37. Mheshimiwa Spika, Kazi zilizotekelezwa zipo katika ukurasa wa 37 hadi 38 katika Kitabu cha Hotuba.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

38. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **Shilingi 11,511,874,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,461,874,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,050,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2019 **Shilingi 4,228,365,695.67** Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 1, 030, 744,696.91** zilipokelewa na kutumika.

39. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 baadhi ya shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

- (i) Jumla ya Viongozi wa Umma 13,945 ambao ni sawa na asilimia 89 kati ya Viongozi 15,937 wamerejesha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2018 ikilinganishwa na Viongozi 15,391 waliorejesha kipindi kama hicho mwaka 2017; na
- (ii) Malalamiko 87 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 60 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi na malalamiko 27 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Uchunguzi wa awali umefanyika kwa malalamiko 60 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, malalamiko 27 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma walalamikaji walipewa ushauri na mengine yalielekezwa kwenye mamlaka zinazohusika.

40. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa zipo katika ukurasa wa 38 hadi 42 katika Kitabu cha Hotuba.

OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA WAKALA ZILIZO CHINI YAKE

3.1.6 Menejimenti ya Utumishi wa Umma

41. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Wakala zake imetekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora, Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

42. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma: Fungu 32 inayojumuisha Wakala zilizo chini yake iliidhinishwa jumla ya Shilingi **41,403,499,261.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **30,464,499,261.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **10,939,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, **Hadi kufikia mwezi Machi, 2019** kiasi cha Shilingi **28,934,685,773.36** zilikuwa zimepokelewa. Jumla ya Shilingi **28,934,685,773.36** zimetumika hadi Machi, 2019.

43. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Pamoja na usimamizi na ufuatiliaji unaofanywa na ofisi kwa watumishi wa umma bado kuna Malalamiko. Katika kipindi hiki jumla ya malalamiko 708 ya ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo yamepokelewa na kufanyiwa kazi;
- (ii) Aidha, Ofisi imesaidia kupatikana kwa watumishi kwa njia ya uhamisho kwa Taasisi mpya 19 zilizoanzishwa;
- (iii) Mapendekezo ya nafasi za uteuzi 1,332 yalipokelewa, kati ya hayo, 1,074 sawa na asilimia 81 yalirejeshwa kwa waajiri baada ya taratibu kukamilika. Aidha vibali vya uteuzi 50 vilitolewa kwa nafasi za uongozi na mikataba ya ajira 74 ilishughulikiwa;
- (iv) Vibali vya ajira mpya na mbadala vyenye nafasi 41,698 kwa kada mbalimbali vimetolewa; sambamba na kupandisha vyeo Watumishi wa Umma 27,439 wa Kada mbalimbali;
- (v) Madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma 34,346 yenye thamani ya Shilingi. 79,855,525,090.03 yamepokelewa baadhi yamehakikiwa na kuidhinishwa na mengine yanaendelea kuhakikiwa. Maelezo yenye takwimu yapo katika taarifa yangu;
- (vi) Ofisi imechambua Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara, Idara zinazojitegemea na kuidhinishwa. Takwimu zipo katika taarifa yangu;
- (vii) Usanifu wa mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) unaoandaliwa na watumishi wa Serikali umekamilika mwezi Desemba, 2018. Ujenzi wa mfumo uliosanifiwa unaendelea. Pia, Maandalizi ya Miradi Mipya ya matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma za Serikali yameendelea kufanyika; na
- (viii) Serikali kupitia Watumishi Housing imekamilisha ujenzi wa nyumba 271 kwa ajili ya kuuza katika Mkoa wa Dar-es-salaam (162), Morogoro (50) na Mwanza (59) Wilaya ya Magu eneo la Kisesa. Ujenzi wa nyumba 92 katika jiji la Dodoma unaendelea.

Aidha, nyumba 7 kwa ajili ya jeshi la polisi katika wilaya mpya ya Nyang'wale Mkoa wa Geita zilikamilika na zipo tayari kukabidhiwa.

44. *Mheshimiwa Spika*, taarifa Kwa kina ya kazi zilizotekelezwa zipo katika ukurasa wa 42 hadi 51 katika Kitabu cha Hotuba.

3.1.7 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

45. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo, ushauri, kufanya utafiti (applied research) na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala. Aidha, Chuo kinaendesha kozi za kitaaluma kwa ngazi za Cheti, Stashahada na Shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji Kumbukumbu, Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Utawala na Manunuzi ya Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo katika Kampasi sita zilizoko kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 pamoja na shughuli nyinginezo za kawaida na za maendeleo kwa muhtasari haya yalifanyika:

- (i) Watumishi wa Umma 536 walipatiwa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma. Vile vile, watumishi 1,980 wamepatiwa Mafunzo yahasuyo Uongozi na Maendeleo; pamoja na Menejimenti na Usimamizi wa ofisi katika taasisi za umma. Aidha, mafunzo ya Awali yalitolewa kwa Watumishi wa Umma wapatao 515. Pia, hamasa kwa waajiri ilitolewa kuwasisitiza kupeleka watumishi kupata mafunzo ya awali mara baada ya kuajiriwa.

46. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine za Chuo zilizotekelezwa zipo katika ukurasa wa 51 hadi 54 katika Kitabu cha Hotuba.

3.1.8 Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

47. *Mheshimiwa Spika*, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) ina jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma na Sekta binafsi kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalum ya muda mfupi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

48. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao imewezesha mafunzo, midahalo na mikutano kazi kwa njia ya video.

49. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyinginezo zilizotekelezwa na wakala zipo katika ukurasa wa 54 hadi 55 wa Hotuba yangu.

3.1.9 Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)

50. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Wakala imetekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Wakala ya Serikali Mtandao ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imefanikiwa kuongeza Taasisi za Umma zilizounganishwa kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Mapato ya Serikali (GePG) kutoka Taasisi 28 zilizotolewa taarifa kwenye bunge lililopita la bajeti mpaka Taasisi 355 zinazojumuisha TANESCO (LUKU), TRA, TPA, EWURA;
- (ii) Utekelezaji wa Serikali Mtandao umeendelea kuratibiwa kwa kutoa viwango na miongozo ya TEHAMA serikalini ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma na kuhakikisha usalama wa mawasiliano. Vile vile, Sheria ya Serikali Mtandao iko katika hatua za mwisho za uidhinishaji serikalini;
- (iii) Mifumo mikubwa ya TEHAMA imetengenezwa kwa Taasisi za Umma kwa lengo la kuboresha utendaji kazi, kuboresha utoaji huduma kwa umma, kurahisisha ukusanyaji wa mapato na kuondoa mianya ya rushwa; na
- (iv) Ili kuwezesha Serikali kuweza kuwa na mawasiliano ndani na nje ya Mji wa Serikali Dodoma, Wakala imeanza ujenzi wa Kituo cha Usaidizi wa Masuala ya Serikali Mtandao kwenye eneo hilo. Kituo hiki kitakuwa kitovu cha mawasiliano pamoja na kulinda usalama wa mifumo na mitandao kwenye mji wa Serikali.

51. Mheshimiwa Spika, Kazi nyingine zilizotekelezwa na e-GA zipo katika ukurasa wa 56 hadi 59 wa Hotuba yangu.

3.2 SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

52. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19 Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma ilitengewa **Shilingi 3,641,184,299.24**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,677,678,299.24** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 1,264,506,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 750,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2019 **Shilingi 957,703,699.24** za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika na **Shilingi 735,375,000** zimetumika kulipia Mishahara. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 122,360,000** zilipokelewa na kutumika.

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imetekeleza kwa muhtasari yafuatayo:-

- (i) Ofisi ilipokea vibali 107 na kuvishughulikia. Aidha, Ofisi imekamilisha kujenga mfumo wa maombi ya kazi kwa njia ya Kielektroniki ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mfumo wa kupanga nafasi za kazi kwa waombaji waliofaulu kwenye usaili wa ana kwa ana (Placement Management Information System). Kukamilika kwa mfumo huu kutapunguza muda wa usaili kutoka siku 52 za sasa hadi siku 45.

54. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa zipo katika ukurasa wa 60 hadi 63 wa Hotuba yangu.

3.3 OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

55. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha 2018/19, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 4,403,479,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,919,493,000 zilikuwa za Mishahara na Shilingi 2,483,986,000 zilikuwa za Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2019 kiasi cha Shilingi 2,917,064,635 za Matumizi ya Kawaida zilikuwa zimetolewa na HAZINA. Kati ya hizo Shilingi 1,211,987,549.94 zilikuwa kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 1,705,077,085.06 ni za Matumizi Mengineyo

56. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Tume imetekeleza majukumu yafuatayo kwa sehemu:-

- (i) Ukaguzi wa kawaida umefanyika katika Taasisi 33 kati ya Taasisi 150 zilizopangwa kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2018/19 sambamba na Ukaguzi maalumu katika Taasisi sita (6); na
- (ii) Tume imefanyia kazi na kutolea uamuzi rufaa 117 na malalamiko manne (4) ya Watumishi wa Umma. Aidha Sekretarieti ya Tume ilihitimisha malalamiko 313 ya Watumishi wa Umma;

57. Mheshimiwa Spika, kazi nyinginezo zilizotekelezwa zipo katika ukurasa 63 hadi 65 wa Hotuba yangu.

3.4 BODI YA MISHAHARA NA MASILAHU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

58. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa fedha 2018/29, Bodi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 1,652,435,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,012,817,000 zilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 639,618,000 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, Bodi imepokea jumla ya Shilingi 832,178,368.38. Kati ya fedha hizo Shilingi. 559,379,600 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 272,798,768.38 kwa ajili ya mishahara.

- (i) Bodi imefanya Utafiti wa hali ya Masilahi katika Utumishi wa Umma na mifumo ya upimaji utendaji kazi. Utafiti huo umehusisha sampuli ya taasisi 130 kati ya taasisi 474 ambazo zimegawanyika katika makundi mbali mbali; na
- (ii) Taarifa ya Tathmini ya Kazi na Uhuishaji wa Madaraja katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2015 hadi 2017, imewasilishwa katika ngazi ya juu Serikalini mwezi Disemba 2018 kwa hatua zaidi.

59. Mheshimiwa Spika, kazi nyinginezo zilizotekelezwa zipo katika ukurasa wa 65 hadi 67 wa Hotuba yangu.

3.5 OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

60. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Fungu 4: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 8,148,504,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,969,632,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 5,178,872,000** kwa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2019, **Shilingi 1,575,186,000** zilipokelewa na kutumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 725,245,500** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 818,366,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 31,575,000** kwa Miradi ya Maendeleo.

61. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Idara ya Kumbukumbu imetekeleza shughuli zifuatazo kwa muhtasari:-

- (i) Mfumo wa utunzaji Kumbukumbu za Kiutendaji umewekwa katika Taasisi za Umma 23. Aidha, Ukaguzi wa mfumo wa utunzaji Kumbukumbu za kiutendaji umefanyika katika Ofisi kumi na moja (11) za Wakuu wa Mikoa.
- (ii) Uwekaji wa mfumo wa kielektroniki wa masijala (e-file system) katika Taasisi za Umma umefanyika. Jumla ya Taasisi za Umma saba (7) zimeunganishwa na kuanza kutumia mfumo huo wa kielektroniki wa masijala; na
- (iii) Uimarishaji katika mfumo wa kielektroniki umefanyika katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Taifa kwa kuingiza kumbukumbu na nyaraka katika mfumo wa kidijitali wa kuhifadhi Nyaraka (Digital Records Management and Preservation System) ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi umefanyika. Jumla ya Mikataba 3,100 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango imefanyiwa "scanning". Aidha, mikataba 2,700 imefanyiwa uhakiki kwa ajili ya kuingizwa kwenye mfumo wa kidijitali wa kuhifadhi Nyaraka.

62. Mheshimiwa Spika, kazi nyinginezo zilizotekelezwa zipo katika ukurasa wa 67 hadi 73 wa Hotuba yangu.

B. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2019/20 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA

63. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, sasa naomba kutoa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

64. Mheshimiwa Spika, Mipango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa Mafungu yafuatayo 20; 30; 32; 33; 67; 94; 09 na 04 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Mwaka 2015 ya Chama Tawala, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatia kama yalivyoainishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

65. Mheshimiwa Spika, Vile vile, Mipango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 imezingatia utatuzi wa changamoto katika utoaji huduma kwa umma kwa

kadri inavyowezekana. Kwa ujumla changamoto hizo ni kama ifuatavyo: Baadhi ya ofisi za utoaji huduma kutokuwepo katika mikoa yote ya Tanzania; Bado kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi juu upatikanaji wa huduma zitolewazo na Taasisi za Umma, kuendelea kuwepo na kaya maskini, ushirikiano mdogo wa wananchi katika suala la utoaji wa ushahidi mahakamani dhidi ya watuhumiwa wa rushwa; kukosekana kwa sheria ya kuwabana wahusika wanaoshindwa kutekeleza ushauri wa TAKUKURU kuziba mianya ya rushwa katika maeneo yao; na Mabadiliko ya TEHAMA yamekuwa yakiibua changamoto katika upelelezi.

1.1. OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

66. Mheshimiwa Spika, Kazi zilizopangwa kwa mwaka 2019/20 kwa fungu 20 na 30 zipo katika ukurasa wa 75 hadi 88 wa kitabu changu cha Hotuba.

4.1.1. Ikulu

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza baadhi ya kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kikanda, Kimataifa na maeneo mengine;
- (ii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
- (iii) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano mikuu ya maamuzi ya Serikali; na
- (iv) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

4.1.2. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

68. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, TAKUKURU imepanga kutekeleza baadhi ya kazi zifuatazo:-

- (i) TAKUKURU itaendelea kuimarisha vita dhidi ya rushwa kwa kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa zilizoanzishiwa kazi pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza. Vile vile, nguvu itawekwa katika uendeshaji wa kesi 416 zinazoendelea na mpya zitakazofunguliwa Mahakamani;
- (ii) Mikakati zaidi itawekwa kwa kushirikiana na wadau ili kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo; na
- (iii) Kujenga majengo ya ofisi za TAKUKURU katika mikoa na wilaya.

4.1.3. TAASISI YA UONGOZI

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza baadhi ya kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa mafunzo ya “Stashahada ya Uzamili ya Uongozi” (Post Graduate-Diploma in Leadership), kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kuimarisha sifa binafsi za kiongozi;
- (ii) Kutekeleza Programu ya kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu majadiliano ya mikataba yenye thamani kubwa; na
- (iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya Uongozi na Maendeleo Endelevu, kutokana na mahitaji na maombi ya walengwa. Kozi 13 zitatolewa.

4.1.4. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

70. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, MKURABITA imejipanga kutekeleza baadhi ya kazi zifuatazo:

- (i) Kuanzisha Vituo vitano vya Urasimishaji Biashara ili kuwawezesha wafanyabishara kupata huduma muhimu sehemu moja katika Halmashauri za Wilaya Tano za Kahama, Tabora, Nyamagana, Songea na Babati. Aidha, mafunzo ya kurasimisha na kuendesha biashara yatatolewa kwa wafanyabishara 5,000 kwa lengo la kuwawezesha kusajili biashara zao;
- (ii) Kuanzisha Kituo kimoja cha urasimishaji wa biashara Zanzibar, katika Manispaa ya Mjini, Mkoa wa Magharibi ili kuwawezesha wafanyabiashara kupata huduma muhimu sehemu moja ambapo wafanyabiashara 1,000 watapata mafunzo na kusajili biashara zao;
- (iii) Kukamilisha urasimishaji wa ardhi mjini katika Halmashauri za Miji ya Morogoro, Tunduma, Babati, Iringa, Arusha, Njombe na Miji Midogo ya Tandala na Ikonda Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa ardhi mjini utafanyika Chakechake na Unguja Mjini. Jumla ya Hati Milki 6,500 zitaandaliwa na kutolewa;
- (iv) Kukamilisha uandaaji na utoaji wa Hati Miliki za Kimila 11,766 kwa wananchi katika Halmashauri za Wilaya za Rufiji, Musoma, Butiama, Chamwino, Nyang’wale, Makete, Mpwapwa, Bukoba Vijijini na Newala za Tanzania Bara. Aidha, urasimishaji wa ardhi vijijini utafanyika katika eneo la Chanjamjawiri Wilaya ya Chakechake Pemba na Mahonda Wilaya ya Kaskazini B Unguja ambapo Hati Miliki 2,000 zitaandaliwa na kutolewa;

- (v) Kukamilisha ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji katika Halmashauri za Wilaya saba ambazo ni Chamwino (vijiji 2), Itigi (kijiji 1), Mbarali (kijiji1), Mbinga (kijiji 1), Mpwapwa (kijiji 1), Mvomero (kijiji 1), na Nachingwea (vijiji 3). Aidha, ujenzi wa Masjala za Ardhi za vijiji viwili utanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala; na
- (vi) Kuendelea na urasimishaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini katika maeneo ya Mkoa wa Geita.

4.1.5. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

71. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, TASAF imejipanga kutekeleza baadhi ya kazi zifuatazo:

- (i) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza ya Mpango. Zoezi hili linategemea kuzifikia kaya za walengwa zipatazo 355,000;
- (ii) Kutoa ajira za muda kwa jumla ya kaya za walengwa 292,188 ambazo zitahusika katika utekelezaji wa miradi 2,640 ya kutoa ajira za muda itakayoibuliwa na jamii. Walengwa hawa watatoka katika Halmashauri 44 pamoja na Unguja na Pemba;
- (iii) Miradi 134 ya afya, elimu, maji, ujasiriamali na barabara za vijijini itatekelezwa chini ya Mpango wa Kuendeleza Miundombinu katika Halmashauri 134. Wawezeshaji 804 watapeleleza mafunzo juu ya namna ya kutekeleza na kusimamia miradi. Aidha, miradi 160 itatekelezwa katika Halmashauri 13 za Mikoa ya Arusha na Njombe kupitia program inayofadhiliwa na Taasisi ya Maendeleo ya Mataifa Yanayozalisha Mafuta kwa Wingi Duniani (OPEC); na
- (iv) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa, uendeshaji na utoaji wa taarifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mpango hususan kuimarisha mawasiliano kati ya maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu Dodoma.

4.1.6. WAKALA WA NDEGE ZA SERIKALI

72. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ndege za Serikali ambao ulikuwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ulianzishwa rasmi tarehe 17 Mei 2002 kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali Namba 3 ya mwaka 1997. Aidha kwa sasa Wakala umehamishwa kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwenda Ofisi ya Rais, Ikulu tarehe 23 Aprili, 2018 kwa Tangazo la Serikali Namba 252 (GN 252) la tarehe 8 Juni, 2018 Wakala ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Wakala ilianzishwa ili kuboresha huduma na

kuimarisha usalama wa usafiri wa ndege kwa viongozi wanaotumia huduma hizo. Aidha, Wakala imeongezewa jukumu lingine la kuratibu kwa niaba ya Serikali, ununuzi wa ndege, kuzikodisha kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege hizo.

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Wakala ya Ndege za Serikali imepanga kutekeleza shughuli mbali mbali chini ya ofisi yangu kama ilivyo kwenye kitabu cha Hotuba

74. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2019/20, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba **Shilingi 23,144,913,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba **Shilingi 564,312,423,717** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 410,123,039,000** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 154,189,384,717** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

1.2. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZILIZO CHINI YAKE

75. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kwa mwaka 2019/20 kwa ukamilifu kwa Fungu 32 zipo katika kitabu cha Hotuba ukurasa wa 89 hadi 102.

4.2.1. Menejimenti ya Utumishi wa Umma

76. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika mwaka wa fedha 2019/20 itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa. Aidha, Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali.

77. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza baadhi ya kazi zifuatazo:-

- (i) Kufanya mapitio ya Sheria na Miongozo mbalimbali ya kiutumishi katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha utendaji kazi.
- (ii) Kuendelea kupokea na kushughulikia mapendekezo ya nafasi za uteuzi, mikataba ya ajira na vibali vya kukaimu nafasi za uongozi kadili maombi hayo yatakavyokuwa yanawasilishwa na waajiri mbalimbali;
- (iii) Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma ambapo katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 44,807 wa kada ya Elimu (13,526), Afya (9,467), Kilimo, Mifugo na Uvuvi nafasi (2,141) Jeshi la Polisi (3,725), Magereza (685), Jeshi la Zimamoto na Uhamiaji (500) na

Hospitali za Mashirika ya Kidini na hiari (1,262). Aidha, Serikali inatarajia kuajiri watumishi 13,002 wa nyinginezo wakiwemo wahadhiri wa vyuo vikuu vyote vya umma nchini. Vile vile, watumishi 290,625 wa kada mbali mbali watapandishwa vyeo kulingana na maelekezo yatakayotolewa;

- (iv) Kuchambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara ya Watumishi wa Umma 21,683 yenye thamani ya Shilingi 50,759,540,017.25 na kuchukua hatua ipasavyo;
- (v) Kuhakikisha kuwa taarifa za watumishi zinakuwa sahihi na kuboresha taarifa za kiutumishi na mishahara kupitia HCMIS
- (vi) Kuhuisha miundo na mgawanyo wa Majukumu ya Ofisi/Wizara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma 100 na kuziwasilisha kwa Mh. Rais kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji; - Lengo ikiwa ni kuongeza ufanisi katika utoaji huduma pamoja na kupunguza ukubwa na matumizi ya Serikali ili fedha zitakazopatikana zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo;
- (vii) Kufanya tathmini na kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA katika taasisi za Serikali ili kuwawezesha kujenga, kusimamia na kuendeleza mifumo ya TEHAMA ya Serikali;
- (viii) Kukamilisha ujenzi wa mfumo mpya wa HCMIS, kutoa mafunzo kwa watumiaji na kuusambaza katika taasisi za Serikali;
- (ix) Kuziwezesha Taasisi za Umma kuandaa na kutekeleza Mikataba ya Utendaji Kazi;
- (x) Kuanza utekelezaji wa Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma kwenye maeneo ya matokeo ya Motisha na Uwajibikaji; Michakato ya Utoaji Huduma; na Menejimenti ya Rasimaliwatu. Pia, tutaendelea kuratibu maandalizi na utekelezaji wa Programu ya Digital Tanzania na vituo vya HUDUMA PAMOJA kwa ajili ya kutolea Huduma za Serikali sehemu moja
- (xi) Kuendelea kuratibu fursa za mafunzo yanayotolewa na wafadhili wa Serikali na Wadau wa Maendeleo kwa mwaka 2019/20; na
- (xii) Kupitia Watumishi Housing miradi ya ujenzi wa nyumba 500 katika mikoa mbalimbali itatekelezwa, ambapo nyumba 300 zitajengwa jijini Dodoma. Aidha, Serikali kupitia Watumishi Housing imepewa fedha na vifaa vya kisasa vyenye thamani ya shilingi Bilioni 1.5 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya upimaji ardhi katika wilaya mbalimbali kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa bei nafuu.

4.2.2. Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

78. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 Chuo kinatarajia kutekeleza baadhi ya malengo yafuatayo:

- i) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa Watumishi wa Umma 1,720. Katika kufanikisha zaidi suala hili natoa rai kwa waajiri wote kutenga fedha na kupeleka watumishi kwenye mafunzo hayo ili kuwa na utumishi bora wa Umma;
- ii) Kufanya miradi ya maendeleo ya kuboresha kampasi mbali mbali kwa ajili ya kuongeza uwezo na ubora wa kutoa huduma za mafunzo na ushauri katika Utumishi wa umma.

4.2.3. Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

79. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao itaendelea kutoa huduma za maunganisho ili kurahisisha huduma za Mafunzo na kupunguza gharama ili kufikia watanzania wengi zaidi kwa muda mfupi iwezekanavyo.

4.2.4. Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)

80. Mheshimiwa Spika, Hotuba yangu imeambatanishwa na mafanikio mengi sana katika eneo la Serikali mtandao. Katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2019/20, Wakala ya Serikali Mtandao katika kuboresha utoaji huduma kwa umma inatarajia kutekeleza baadhi ya kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa msaada wa kiufundi na kujenga uwezo wa Taasisi za Umma katika kutengeneza na kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato na maduhuli ili iweze kusomana na mfumo mkuu wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato serikalini (GePG);
- (ii) Kuendelea kuongeza uwezo wake kwa Mifumo na miundombinu shirikishi ya ya TEHAMA Serikalini na kuimarisha taratibu za kiusalama;
- (iii) Kufanya utafiti, kuhamasisha ubunifu na maendeleo ya Serikali Mtandao kupitia Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Maendeleo ya Serikali Mtandao cha muda kilichopo Chuo Kikuu cha Dodoma. Vile vile kujenga kituo kikubwa cha kuratibu shughuli hizo; na
- (iv) Kukamilisha kituo cha Usaidizi wa Masuala ya Serikali Mtandao kwenye mji wa Serikali, Ihumwa, kwa kuweka vifaa vinavyoimarisha mawasiliano kwenye mji huo pamoja na kulinda usalama wa mifumo na mitandao ya mawasiliano.

81. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2019/20 kwa ufanisi, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba kiasi cha **Shilingi 72,572,322,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 31,512,322,000**, ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 41,060,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

1.3. SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

82. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2019/20, baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:

- (i) Kuendelea kupokea Matamko ya Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na madeni yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (ii) Kuchunguza tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 2,000; na
- (iii) Aidha, Kutekeleza miradi ya Maendeleo kwenye uimarishaji wa Huduma za kupokea Matamko ya Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na madeni na Ujenzi wa Ofisi za Kanda na Makao Makuu Dodoma.

83. Mheshimiwa Spika, Kazi nyinginezo zilizopangwa kwa mwaka 2019/20 kwa Fungu 33 zipo katika ukurasa wa 102 hadi 104 wa kitabu cha Hotuba

84. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 9,999,945,900**. kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 7,382,075,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,617,870,900** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

85. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2019/20, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza baadhi ya majukumu yafuatayo:-

- (i) Kusimamia na kuendesha michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;
- (ii) Kuendelea kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar kurahisisha michakato ya ajira kwa ajira za Muungano; na
- (iii) Kuboresha mifumo ya uendeshaji wa usaili kwa kutumia mbinu za kisasa, ikiwemo matumizi ya “psychometric test”.

86. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizopangwa kwa mwaka 2019/20 kwa Fungu hili zipo katika ukurasa wa 104 hadi 105 wa Kitabu cha Hotuba

87. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2019/20, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Shilingi 2,376,443,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

1.4. OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

88. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume imepanga kutekeleza baadhi ya majukumu yafuatayo:-

- (i) Kufanya Ukaguzi wa kawaida katika Taasisi 150 na Ukaguzi Maalum katika Taasisi 10 kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;
- (ii) Kufanya mikutano minne (4) ya kisheria ya Tume kujadili na kutolea uamuzi rufaa, malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakvoyopokelewa;
- (iii) Kuhuisha Miongozo ya Tume ya uzingatiaji wa masuala ya Ajira na Nidhamu na kuisambaza kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu;
- (iv) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/19 na kuiwasilisha kwa Rais;

89. Mheshimiwa Spika, kazi nyinginezo zilizopangwa kwa mwaka 2019/20 kwa Fungu hili zipo katika ukurasa 106 hadi 107 wa Hotuba yangu.

90. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2019/20, Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa jumla ya kiasi cha Shilingi 4,889,606,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

91. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2019/20, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09) inatarajia kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:-

- (i) Kufanya utafiti wa hali ya mishahara na masilahi katika vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo ni Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ili kushauri namna bora ya kutoa motisha kwa kuzingatia viwango stahiki vya kuongeza ufanisi katika kazi za vyombo hivyo; na
- (ii) Kuandaa taarifa 4 za gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mishahara wenye staha; taarifa hizi zinawezesha kushauri kuhusu kiwango cha mishahara unaoendana na gharama za maisha.

92. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyinginezo zilizopangwa kwa mwaka 2019/20 kwa Fungu hili zipo katika ukurasa 107 hadi 108 wa Hotuba yangu.

93. *Mheshimiwa Spika*, Ili kutekeleza mpango huu wa mwaka 2019/20, Fungu 09: Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inaomba kutumia jumla ya **Shilingi 1,474,241,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.**

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

94. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2019/20, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kukusanya taarifa na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya Nchi yetu kutoka Taasisi za Umma na watu binafsi;
- (ii) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Taifa kwa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuingiza taarifa katika mifumo ya kidijitali ya kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka (Digital Records and Archives Management and Preservation Systems) ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi;
- (iii) Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;
- (iv) Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa; na
- (v) Kuanzisha na kuimarisha Vituo vya Kanda kwa lengo la kuongeza uwezo wa Idara katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka kwenye Kanda husika.

95. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zilizopangwa kwa mwaka 2019/20 kwa Fungu hili zipo katika ukurasa wa 108 hadi 110 katika kitabu cha Hotuba yangu.

96. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha wa 2019/20, Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,774,066,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 2,774,066,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.**

C. MAJUMUISHO

97. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi yangu ndiyo inayohusika na uwezeshaji wa maamuzi ya juu ya nchi sambamba na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo wote ni mashahidi kuwa ni mtambuka kwa taasisi zote za Umma. Vile vile, wote

tunajua jinsi ambavyo Utumishi wa Umma ulivyo nguzo muhimu katika uendeshaji wa Nchi na hivyo kutoa mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi inayodhamiria kuwa na uchumi wa Watanzania wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Aidha, maendeleo hayo yanatarajiwa kupatikana kwa kuimarisha uchumi wa viwanda kama inavyowekwa wazi katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

98. Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu itaendelea kuimarisha uwezeshaji wa vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama na kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Maadili kwa viongozi wote na watumishi wa umma yanatarajiwa kuchangia ipasavyo kwenye nchi kupata tija ya rasilimaliwatu na rasilimalifedha kwa kuwa na matumizi yenye tija wakati wote ya rasilimali hizo. Kati ya mambo ambayo Serikali itayapa kipaumbele ni usimamizi thabiti wa maeneo hayo.

99. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa ujumla inafanya maboresho ya kisekta na mtambuka, wajibu wa Ofisi yangu itakuwa ni kuhakikisha maboresho yanayofanywa katika nchi yetu hayana urudufu na yanaleta tija katika Utumishi wa Umma na kuchochea maendeleo. Aidha, itahakikisha kunakuwepo na utawala bora ulio imara kuanzia ngazi ya juu hadi chini ya uongozi. Katika kuimarisha uwazi Ofisi yangu itahakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu Uamuzi wa Serikali kuhusu masuala mbalimbali.

100. Mheshimiwa Spika, kwa nchi yetu na kwa mujibu wa miundo na mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, utekelezaji kwa ujumla unajumuisha, Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

101. Mheshimiwa Spika, Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye eneo la kuimarisha utendaji kazi wa Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio wa lazima katika utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenye masilahi mapana kwa Taifa letu.

102. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, kuzingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu ili kujenga imani zaidi kwa wananchi. Katika kuendana na wakati jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali.

103. Mheshimiwa Spika baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19 na Mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/20, sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi yetu kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

a.	Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu		
	i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	23,144,913,000
	Jumla	Sh.	<u>23,144,913,000</u>
b.	Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri		
	i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	410,123,039,000
	ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>154,189,384,717</u>
	Jumla	Sh.	564,312,423,717
c.	Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma		
	i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	31,512,322,000
	ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>41,060,000,000</u>
	Jumla	Sh	<u>72,572,322,000</u>
d.	Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma		
	i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	7,382,075,000
	ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>2,617,870,900</u>
	Jumla	Sh	<u>9,999,945,900</u>
e.	Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma		
	i. Matumizi ya Kawaida	Sh.	2,376,443,000
	Jumla	Sh.	2,376,443,000
f.	Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma		

	Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>4,889,606,000</u>
	Jumla	Sh.	4,889,606,000
g.	Fungu 09: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma		
	Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>1,474,241,000</u>
	Jumla	Sh	<u>1,474,241,000</u>
h.	Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa		
	Matumizi ya Kawaida	Sh.	2,774,066,000
	Matumizi ya Miradi ya Maendeleo		<u>2,000,000,000</u>
	Jumla		<u>4,774,066,000</u>

104. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2019/20, ni kama ifuatavyo:-

Jumla kuu - Matumizi ya Kawaida	Sh.	483,676,705,000
Jumla kuu - Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>199,867,255,617</u>
Jumla kuu kwa Mafungu yote	Sh.	683,543,960,617

105. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.